Imetayarishiwa na imeandikwa chini ya uongozi wa
Jopo Linalohusika na Kutetea Haki za Wafalastini
ambazo zisizoweza kupokonyeka

# HOJA YA FALASTINI
# HISTORIA FUPI

UMOJA WA MATAIFA
New York, 1980

## YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| | Utangulizi | 1 |
| I. | Falastini katika historia | 2 |
| II. | Ahadi zisizolingana juu ya Falastini | 4 |
| III. | Hukumu iliyotolewa juu ya Falastini | 6 |
| IV. | "Maskani ya kitaifa" na kinzano la Wafalastini | 10 |
| V. | Kupigwa mapande Falastini na kuundwa kwa Israeli | 14 |
| VI. | Masiala ya Falastini katika Umoja Wa Mataifa, 1948-1967 | 19 |
| VII. | Utambuzi wa haki za Wafalastini za kujitawala wenyewe | 21 |

# UTANGULIZI

Sehemu maalumu iliyopewa Falastini katika historia inatokana na umuhimu wa nchi hiyo katika dini tatu tukufu zinazoamini Mungu mmoja. Kwa sababu hii, Falastini inaonesha ni nchi ya amani, lakini, kwa hakika, mazingira ya historia na mara nyingine ya kidini na wakati mwingine ya kisiasa yameleta mapambano na hata nchi yenyewe kutekwa.

Hadi leo, Falastini inaendelea kuwa na ugomvi na mizozo ambayo inasababisha hofu kuu juu ya usalama wa dunia. Mapisi katika karne yetu hii yaliyosabibisha mambo haya ya hatari, mara-kwa-mara hufifirishwa kwa ajili ya mgogoro mkuu juu ya "Suala la Falastini." Utafiti huu mfupi unachungua asili ya suala hilo.*

---

*Maandishi haya ambayo yanashughulika na habari ngumu mno yamekusudiwa wasomaji walio wangali watoto, na taarifa yenyewe imeandikwa kwa mukhtasari kutokana na utafiti mrefu uliochapwa na Umoja Wa Mataifa unaoitwa: The Origins and Evolution of the Palestine Problem - Part I and II (1978) na The Question of Palestine (1979).

## I. FALASTINI KATIKA HISTORIA

Asili ya mgogoro uliopo juu ya Falastini unatokana na maongozi yaliyotolewa wakati Falastini ilipokuwa chini ya himaya ya Shirika La Mataifa ambalo ni asili ya Umoja Wa Mataifa. Taarifa iliyotolewa 1930 na ujumbe* uliochaguliwa na kukubaliwa na Shirika La Mataifa imechungua historia ya kale ya Falastini kwa upeo wa kutokupendelea. Yanayofuata ni mukhtasari wa taarifa hiyo.

Katika zama za zama, Falastini ilikaliwa na makundi ya Wasamiti, na katika hao, walioishi hapo na mapema zaidi walikuwa Wakanaani. Kwa mujibu wa mapokezi, Nabii Ibrahimu, ambaye ni mzazi wa asili wa Mayahudi na Waarabu, alitoka Uru kabla ya kukaa Kanaani.

Makabila ya Waisraeli yalipowasili Falastini baada ya kutoka uhabusini katika nchi ya Misri, yaliungamanishwa na Mfalme Daudi yakawa katika mamlaka mamoja mnamo miaka 1000 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu (1000 K.Y.). Mamlaka hayo yalifika upeo wa taadhima wakati alipotawala mtoto wa Mfalme Daudi, yaani Sulemani, ambaye alijenga jumba la kwanza la ibada la Jarusalemu juu ya mlima wa Moraya. Lakini, baada ya kifo cha Sulemani, historia ya watu wa Israeli--au tuseme ile ya mamlaka mbili ya Israeli na Judia--ni hekaya ya vita na mapambano baina ya wenyewe kwa wenyewe na baina yao na makabila mbali nao.

Mnamo mwaka 720 K.Y., Waasiria waliangamiza ufalme wa Israeli na wakawateka wakaazi wake. Mnamo miaka ya 600 K.Y., Mfalme Nibuchadenezari wa Babiloni alihujumu mamlaka ya Juda, na katika mwaka 567 K.Y., akabomoa Jarusalemu pamoja na Jumba la ibada la Sulemani. Takriban wakaazi wote walitekwa. Miaka hamsini baadaye Mfalme Sairusi wa Ajemi (Fursi) alipoiteka Babiloni, ndipo Mayahudi walipoweza kurudi Falastini. Mnamo mwaka 515 K.Y., walilijenga tena Hekalu la Sulemani.

Katika mwaka 332 K.Y., Mayahudi walishindwa nguvu na Wamasedonia na wakakutishwa taabu. Takriban mwaka 170 K.Y., Mayahudi walijaribu kuleta mapinduzi lakini hawakufauli, na hekalu la pili pia likabomolewa. Baada ya utawala wa Wamasedonia kumalizika, kulipatikana na uhuru wa kadiri fulani. Uhuru huu uliendelea mpaka Pompei wa Urumi alipoteka na kuingia Jarusalemu katika mwaka 63 K.Y. Katika mwaka 70 Baada ya Yesu (B.Y.), Titus aliubomoa mji huo. Hapana kilichobakia katika Hekalu la pili ila Ukuta wa Magharibi ambao ulikuja kujulikana kwa jina la Ukuta Wa Maombolezi.

---

*Wanajopo wa ujumbe huo walitoka Nadhalendi, Swideni na Swizalendi.

Mwanzoni mwa karne ya pili B.Y., Mfalme Hadriani aliwapiga marufuku Mayahudi kuingia Jarusalemu. Kutoka wakati huo Mayahudi walianza kutawanyika katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kutoka hapo hadi kuanzishwa kwa taifa la Israeli mnamo mwaka wa 1948, hakujakuwepo na serikali ya Kiyahudi katika Falastini wakati wote huo, idadi yao ilipanda na kushuka kwa mujibu wa mapendekezo ya mtawala anayetawala wakati fulani.

Baada ya kugawanywa mamlaka ya Urumi katika mwaka wa 400 B.Y., Falastini iliingia chini ya utawala wa Bizantiamu hadi Waarabu walipoiteka katika mwaka wa 637 B.Y. Juu ya sehemu ilowahi kuwa Hekalu la Sulemani ambayo imetupwa na kuwa gofu, Msikiti wa Aqsa na Kuba la Jabalini lilijengwa na kuitwa Haram el-Sharif. Msikiti huo ni mtakatifu sana kwa Waislamu na ni wa pili kwa utukufu kufuatia Maka na Madina.

Katika kipindi cha shuwari baina ya vita vya Waislamu na Wakristo, mnamo mwaka wa 1099 hadi 1190 Salahadini, mtawala wa Waarabu, aliwaita na kuwakaribisha Mayahudi kurudi Falastini.

Mnamo mwaka wa 1517, Waturki waliiteka nchi na kuitawala mpaka mwisho wa vita vya Kwanza vya Dunia. Katika wakati wote huo, ukuta wa Maombolezi, uliendelea kuwa mahala pa ibada kwa Mayahudi.

Mwishoni mwa mwaka wa 1917, majeshi ya Uingereza yaliteka Falastini.

Tukiitoa ile miaka michache waliyotawala Wakristo waliopigana vita vya msalaba, ni wazi kuwa Falastini ilimamlikiwa na Waarabu na baadaye na Waturki kwa muda wa miaka zaidi ya 1,300 kuanzia mwisho wa utawala wa Wabizantiamu. Wengi zaidi ya watu wa Falastini walikuwa Waislamu na baadhi yao Wakristo. Pia palikuwa na idadi ndogo ya Mayahudi wa kabila la Kisamiti. Waarabu na pia Waturki wa dola la Kiathumani waliwapa Mayahudi haki za kuendelea kuabudu na kustawisha hisi zao za kidini juu ya Falastini. Katika karne ya kumi na tisa, wakati ambao baadhi ya nchi za Ulaya (Uropa) ambako ugozi dhidi ya Wasamiti ulikuwa unazidi kila siku Waathumani waliruhusu makundi madogomadogo ya wahamiaji wa Kiyahudi kufanya makaazi yao Falastini. Katika 1917 walipokuwa Waingereza ndio wanaotawala idadi ya Mayahudi katika Falastini ilikuwa kasoro ya asilimia kumi. Tisa katika kila watu kumi walikuwa Waarabu; Waislamu (asilimia 80) na Wakristo (asilimia 10). Mila, dasturi na lugha ya Waarabu wa Falastini ilikuwa ndiyo utamaduni wenye nguvu zaidi.

## II. AHADI ZISIZOLINGANA JUU YA FALASTINI

Katika Vita Vya kwanza Vya Dunia, Uingereza na waloungana nao walikuwa wakitafuta muawana katika mapambano yao na Wajarumani walioshirikiana na Dola la Waathumani. Kwa sababu wakati huo baadhi ya wakuu wa Waarabu walikuwa wakitaka kujigomboa na utawala wa Kiathumani, usuhuba baina ya Waingereza na Waarabu haukuwa na budi. Hatimaye, katika 1915 palipatikana makubaliyano fulani baina ya Sharifu wa Maka, aliyekuwa akipatana kwa niaba ya Waarabu, na Sir Henri Mekmahon aliyekuwa kamishna Mkuu wa Misri aliyewakilishwa kuwa msemaji wa Uingereza. Sharifu huyo alidai ikubaliwe kuwa nchi za Waarabu zote pamoja na Falastini zilioko chini ya himaya ya Waathumani kuwa ni nchi huru. Lakini, Mekmahon alijaribu kuipiga pande Falastini kwa kutokueleza sawasawa ni ardhi gani watazokubali kuzitambua kuwa ni huru. Sharifu huyo alipinga mipango ya Mekmahon. Mzozo uliendelea hadi 1939 wakati ambao Waingereza walipokiri kuwa katika 1917 "hawakuwa na nguvu za kuigawa Falastini."

Kwa hakika, mkataba wa Sykisi-Pikot wa 1916, mkataba wa siri baina ya Waingereza na Wafaransa unaohusikana na uhuru wa Waarabu, uliipiga pande Falastini isipate uhuru, na badali yake walitaka iwe chini ya "uwakili wa mataifa."

Uamuzi juu ya mustakabali wa nchi ya Falastini ulikua pia jambo waliloahidiwa Chama Cha Wazayonisti Wa Dunia na serikali ya Kiingereza. Katika mwaka 1897, Chama hicho kilitangaza lengo lake la "kuwaundia Mayahudi makao ya uwananchi ambayo yatakayothibitishwa na sheria za nchi. Chini ya uongozi wa Theodor Herzeli, Chama hicho kiliangalia pia sehemu fulani za Afrika ya Mashariki na Ajentina katika kutafuta mahala panapofaa kuweka makao yao ya uwananchi. Hatimaye, Chama hicho kiliamua kuweka makao yao Falastini kwa sababu ya uhusiano wa kale wa Mayahudi na ardhi hiyo takatifu.

Viongozi wa Kizayonisti walijitahidi katika kutafuta muawana kutokana na Serikali ya Kiingereza; walitia mkazo juu ya umuhimu kwa Waingereza wa kuwa na mwawini mpya ambaye atasaidia kuhami mfereji wa Suezi. Waingereza ambao bado walikuwa wakitafuta auni juu ya juhudi zao za vita vilivyowakabili, walikubaliana na Wazayonisti. Basi, Katibu Wa Mambo Ya Nje, Lodi Belfo, aliwaandikia barua, tarehe 2 Novemba 1917, Chama Cha Wazayonisti Wa Dunia. Barua hii, ambayo ilikuja kujulikana kama Ilani Ya Belfo, ilinena yafuatayo:

> "Serikali ya Mtukufu Mfalme inakubaliana na jambo hili la kujengwa maskani ya uwananchi ya Kiyahudi katika Falastini, na itafanya kila bidii ili kuhakikisha kupatikana lengo hili, lakini ijulikane wazi

kwamba kisitendwe chochote ambacho kitaharibu ukaazi na haki za kidini zilioko za watu wasiokuwa Mayahudi katika Falastini au haki na vyeo vya kisiyasa walivyovishika Mayahudi katika nchi nyingine yoyote ile."

Baadhi ya umati za Mayahudi zilihisi kuwa huenda pakazuka hisiya za utiifu zenye kupingana na uraia wa nchi zao, walipinga mipango ya Wazayonisti. Sar Eduwadi Montagu, aliyekuwa yeye peke yake Myahudi katika Baraza la Mawaziri la Uingereza, aliponda vikali mipango hiyo. Hata Daktari Shaimu Waizameni, kiongozi wa Wazayonisti aliandika yafuatayo, miaka kumi tu baadaye:

> "Ilani ya Belfo ya 1917 iliundwa juu ya hewa . . . kila siku na kila saa katika miaka kumi hii iliyopita, tunapofungua gazeti, nilidhani: Wapi kutazuka dharubu nyingine? Nilikhofu isije Serikali Ya Kiingereza ikaniita na kuniuliza: 'Tuambie, ni nini hichi Chama Cha Wazayonisti? Wako wapi, hao Wazayonisti wako?' . . . Waingereza walijua kuwa Mayahudi walikuwa dhidi yetu: Tulikuwa peke yetu juu ya kisiwa kidogo, kundi dogo la Mayahudi ambao tuliokuwa na asili ya kigeni."

Ili kutangua ukinzani wa Waarabu juu ya mipango hiyo mipya. Ilani mpya ya Waingereza na Wafaransa ilikariria ahadi walizowapa Waarabu juu ya uhuru kamili. Taarifa ya tarehe 7 Novemba 1918 iliwahakikishia Waarabu juu ya "Uhuru thabiti na kamili . . . na kuimarisha serikali ya kidola na utawala ambao utahalalishwa kutokana na juhudi na kwa khiyari zao wazalendo."

Juu ya ahadi zilizotolewa katika Taarifa ya tarehe 7 Novemba, Matokeo yaliyofuata ya Falastini yalidhihirisha kuwa walivyotaka wengi ya watu wa Falastini yawe, hayakuwa na nguvu. Nchi yao iliahidiwa kupewa watu wengine na Serikali ya kigeni ambayo, katika wakati huo, Serikali hiyo haikuwa na haki yoyote ya kimamlaka Falastini. Wakiangalia mambo haya, mabingwa wengi walithibitisha kuwa Ilani Ya Belfo haikuwa na uthibiti au haki katika sheria isipokuwa ilikuwa ni maneno ya serikali fulani yanayoonesha namna inavyopendelea.

## III. HUKUMU ILIYOTOLEWA JUU YA FALASTINI

Taarifa ya Belfo ilipewa taadhima katika dunia kwa sababu ilifanywa kuwa ni sehemu ya Hukumu Iliyotolewa Juu Ya Falastini. Hiyo Hukumu yenyewe ilitokana na mapatano yasiyokuwa na budi baina ya ubeberu uliokuwepo wakati huo na kanuni za kuendesha mustakabali kwa mujibu wanavyotaka watu wenyewe, watu waliokuwa chini ya utawala wa kigeni--kanuni zenyewe zilitolewa na Rais Wudro Wilson. Baada ya Waingereza na washirika wao kushinda Vita Vya Kwanza Vya Dunia, mipango ya Hukumu ya Shirika La Mataifa iliwatia wengi ya wale watu waliokuwa chini ya mamlaka ya Waathumani, Wajarumani na Waaustro-hangeriani chini ya utawala wa washindi fulani. Lengo la Hukumu lililowekwa wazi ni kuwaongoza watu walotawaliwa hadi kupata uhuru wao.

Kulikuwa na babu tatu za Hukumu ambazo daraja zake zilitafautiyana kwa kutegemea hisiya ya dola zilizoshinda vita juu ya maendeleo ya kisiyasa ya watawaliwa. Nchi zote za Waarabu zilizokuwa chini ya mamlaka ya Waathumani, pamoja na Falastini, ziliwekwa kwenye daraja ya juu kabisa. Mikataba ya Shirika La Mataifa ilieleza kuwa wale watu waliokuwa katika daraja hii ni wale ambao "kuwa kwao huru kunaweza kukubaliwa mara moja," na huku wakisaidiwa katika mambo ya "kutawala na kupewa nasaha." Suuria na Lebanani ziliwekwa chini ya hukumu ya Wafaransa, na Falastini na Jodani Kuu zilitiwa chini ya hukumu ya Waingereza. Kwa kufuata mikataba juu ya kuwapa watu uhuru wao, nchi hizo mbili zilizokuwa zikihukumiwa na Wafaransa zilipata uhuru kabla ya mwisho wa Vita Vya Pili Vya Dunia. Uhuru wa Lebanani ulipatikana Novemba 1943 na kufuatiwa na Suuria katika January 1944. Jodani ilipata uhuru 1946. Lakini, Falastini ilikuwa mahala pa mapambano.

Mikataba ya Shirika La Mataifa iliamua kuwa matakwa ya jamii za watu wanaohusikana na mambo haya yawe ndio sababu kubwa ya daraja watakayowekwa. Lakini haya yaliwekwa upande tukiangalia kisa cha Falastini.

Katika mkutano Wa Amani Wa Parisi wa 1919, Rais Wilson alishikilia, mpaka ukawekwa ujumbe ili kuchungua matakwa ya wananchi wenyewe. Ujumbe huo ulipendelea zaidi Hukumu ya Wamarekani kuhusu Suuria pamoja na Falastini. Baada ya kuchungua hisiya za wananchi wenyewe wa Falastini kuhusu uhamiaji wa Mayahudi nchini humo, ujumbe ulipendelea kuwa "mipango iliyopindukia mipaka ya Wazayonisti juu ya uhamiaji wa Mayahudi Falastini irakibishwe kikweli." Ujumbe ulitangaza kuwa mipango ya Wazayonisti ambayo ililenga ". . . mwishowe kuifanya Falastini nchi ya Mayahudi peke yao [itakuwa] ni ya haramu kwelikweli. Katika kujadili dai la Wazayonisti "kuwa wao wana 'haki' Falastini, kwa sababu waliwahi kuishi huko miaka elfu mbili iliyopita," Ujumbe ulinena kuwa madai haya

ni shida kuyatia akilini."

Katibu wa Mambo Ya Nje wa Uingereza, Lodi Kuazoni, alihadharisha kuwa haya maneno "maskani ya kitaifa" kwa kusema kweli maana yake ni "dola la Kiyahudi" ambalo litawafanya Waarabu wawe raia duni. Alisema, "ninafikiri kuwa mipango hiyo hakika ni miovu." Belfo Mwenyewe alikiri haya na alinena, "kuwa kwa mujibu wa mambo yanayohusu Falastini, Dola /zilizoshirikiana/ hawakutoa taarifa yoyote ya mambo yalivyo ambayo, kwa kusema kweli, yasiyokuwa ya upotovu, wala hawakutoa ilani ya siyasa ya kiserikali . . . ambayo hawakuwa na lengo la kwenda kinyume nayo.

Alakulihali, mipango iliyopangiwa Falastini ilipelekwa mbele kama dasturi. Mnamo 1920, katika mkutano wa San Remo, Ufaransa ilikubali kuwa iwapo hatua waitakayo juu ya mambo yanayohusu Suuria na Lebanani itachukuliwa, Falastini itakuwa chini ya Waingereza badala ya Umoja Wa Madola kama lilvyopangwa awali. Na zaidi ya hayo, ilani iliyotilia mkazo na iliyoweka mambo wazi zaidi ya ile ya Belfo ilifanywa kuwa sehemu ya Hukumu juu ya Falastini. Na hapo ilipoongezwa sehemu hii mpya, Hukumu ilitambua pia Chama Cha Wazayonisti kuwa ni "Ujumbe Wa Mayahudi" ambao utasaidia kuunda ukaazi wa Kiyahudi kwa kutayarisha misafara mingi ya Mayahudi kutoka ng'ambo ili wahamie Falastini ni kuwatengenezeya mipango ya kuishi katika ardhi ambazo zimenunuliwa na Ujumbe huo.

Ni jambo lenye kugutusha kuona kuwa Hukumu, hata mara moja, haikutaja neno "Mwarabu" ndani yake. Ijapokuwa Waarabu wa Falastini walikuwa ni idadi ya watu tisa katika kila kumi ya watu waliokuwa Falastini wakati huo, lakini, katika waraka walitajwa kwa maneno yasemayo "watu wasiokuwa Mayahudi katika Falastini." Mwandishi mmoja alifananisha matumizi ya maneno haya yenye kinyume cha kuchekesha kuwa ni sawa na "kuita Umati, watu wasiokuwa chembe," na mwandishi huyo alikariria, kweli iliyo dhahiri, kuwa hao waliokuwa na idaki kubwa zaidi sana katika Falastini ni Waarabu. Haki moja tu walipewa umati wa Waarabu, nayo ni ya maneno yasemayo kuwa "kisitendwe chochote ambacho kitaharibu ukaazi na haki /zao/ za kidini." Kutajwa kwa namna yoyote haki zao za kiuwananchi au za kisiasa hakukutajwa na haya yalitendwa bila ya kificho.

Hukumu hiyo ilitiwa sahihi tarehe 24 Julai 1922 na ilianza kufuatwa katika mwezi wa Septemba 1922. Ijapokuwa Jodani Kuu ilikuwa, hapo awali, katika Hukumu hiyo ya Falastini, lakini tarehe 16 Septemba 1922, Chama Cha Mataifa kiliamua kuwa Jodani iendeshwe na uwakili mwingine. Hatimaye, Kukumu ilihusika na Falastini tuu peke yake, ingawaje ardhi zilizodaiwa kufanywa ni za makaazi ya Mayahudi zilivuka nje ya mipaka ya Falastini (angalia Taswira ya 1).

Moja katika lengo la Hukumu lilikuwa "kutayarisha mambo ya kujitawala wananchi wenyewe." Lakini, rai ya Serikali ya Kiingereza

Taswira ya 1




"PALESTINE" CLAIMED BY ZIONIST ORGANIZATION, 1919

(Source: Ruedy in Abu Lughod: The Transformation of Palestine)

iliyotangazwa tarehe 1 Julai 1922, ililifanya lengo hilo kuwa duni. Tangazo ambalo liliitwa "Ilani ya Chachil," liliweka "wazi kuwa kutayarishwa kwa mambo ya kujitawala wanachi wenyewe katika Falastini yawekwe upande na badali yake ahadi muhimu kabisa na wajibu uliotupasa kuwaundia Mayahudi makaazi ya Kiuwananchi katika Falastini iwekwe mbele.

Mambo yenye kupingana katika Hukumu moja hiyo ilifanya Hukumu hiyo kuitwa "budi mbili" juu ya Chama Cha Wazayonisti na Waarabu wa Falastini. Hizi "budi mbili" zilikuwa zinapingana na hatimaye kuleta ugomvi baina ya wananchi wa Falastini na wageni wanaohamia huko kutafuta pa kupumua, kukimbia ugozi uliokuwa Ulaya.

## IV. "MASKANI YA KITAIFA" NA KINZANO LA WAFALASTINI

Kuundwa kwa "Makaazi Ya Kiuwananchi" kulianza mapema baada ya Vita Vya Kwanza Vya Dunia--Kabla sana ya Hukumu hiyo kuanza kufuatwa katika 1922. Chama Cha Wazayonisti kilitengeneza mipango ya uhamiaji kwa wingi ya Mayahudi, mipango ambayo ilibadilisha sana idadi na maumbile ya sura za makundi ya watu wa Falastini. Idadi ya Mayahudi katika Falastini ilipanda kutoka 56,000 katika 1918 na kuwa kadiri 88,000 katika 1922, katika idadi ya watu wote iliyokisiwa rasmi kuwa ni 750,000. Hadi kufika 1939, idadi ya Mayahudi ilipanda na kufikia 445,000 kutokana na idadi ya watu wote iliyokuwa milioni moja u-nusu. Kuzidi kwa idadi ya Mayahudi namna hii kulisababishwa zaidi na kukimbia kwao kutokana na ukatili wa Wanatzi.

Tukiangalia kwa hisabu ya asilimia tutaona kuwa idadi ya Mayahudi ilipanda kuanzia asilimia 10 katika 1919 mpaka asilimia 17 katika 1929 na kufikilia asilimia 30 katika 1939 (Taswira ya 2).

Taswira ya 2

Idadi ya Watu Falastini




| 1919 | | 1929 | | 1939 | |
|---|---|---|---|---|---|
| Waarabu | 90% | Waarabu | 83% | Waarabu | 70% |
| Mayahudi | 10% | Mayahudi | 17% | Mayahudi | 30% |

Chama Cha Mayahudi kilinunua pia ardhi ili kuwafanyia maskani wageni wa Kiyahudi waliokuja kuhamia. Katika 1920, ardhi za mayahudi zilikuwa asilimia 2.5 ya ardhi yote ya Falastini. Kufikia 1939, zilizidi hadi kufikilia asilimia 5.7 ya ardhi yote ya Falastini.

Waarabu waliokuwa wananchi wa Falastini waliona kuwa mipango hii ya Wanachama Wa Kizayonisti ya kuongeza idadi ya Mayahudi na idadi ya ardhi wanazozimiliki katika Falastini ni ukoloni wa kigeni juu ya nchi yao ya toka babu-na-mababu. Kwa sababu Wafalastini walikuwa bado hawajaelimika juu ya mipango ya kisiasa, basi hamaki zao walizionesha kwa kufanya mchafuko. Fujo dhidi ya Wazayonisti lilizuka katika 1920, 1921, 1929 na 1939. Serikali ya Kiingereza iliweza kuukandamiza uhalifu kwa kutumia askari wa jeshi na mabavu yaliyopindukia mipaka.

Katika 1937, Ujumbe Wa Kifalme ulioongozwa na Lodi Fiil ulipelekwa Falastini ili kuchungua sababu za michafuko iliotokea. Ujumbe ulitoa maoni yake yaliyosema kuwa kiini cha sababu ya uhalifu na uasi uliotokea kabla ilikuwa kwanza, ni hamu waliyokuwa nayo Waarabu wa Falastini kupata uhuru wao na pili, "chuki zao na hofu juu ya kuundwa kwa makaazi ya kitaifa ya Kiyahudi" katika nchi yao. Zaidi ya haya Ujumbe ulinena kuwa ". . . Kuigeuza Falastini nchi ya Mayahudi kwa kutumia mabavu na kwenda kinyume na hitiyari ya Waarabu . . . hakika ni kutenda kinyuwe cha makusudio na lengo la mpango wa Hukumu. Haya yatakuwa ni kuwakatalia wananchi haki ya kujichagulia mustakabali wautakao wakati Waarabu ndio wenye idadi kubwa katika Falastini na kutoa haki hiyo wakati ambao Mayahudi wamekuwa ndiyo wenye idadi zaidi . . . ."

Na zaidi ya hayo, baada ya kutafiti, Ujumbe umegundua kuwa ugomvi wenyewe haukuwa "kwa hakika, mgogoro wa kigozi unaotokana na chuki za Waarabu juu ya Mayahudi. Kwani hapo kale hapakutokea na mzozo wa aina hiyo . . . mpaka wakati wa mapambano ya Falastini ndipo zilipozalikana chuki hizo." Ujumbe ulinena kuwa dini ya Kiyahudi na ibada zake zilikuwa zimetia mizizi katika kale ya Falastini na kuwa baadhi ya Mayahudi walikuwa wakiishi huko siku zote. Kwa hakika mgogoro umetokana na Wafalastini kukana Ilani Ya Balfoo na Kupinga mipango ya Wazayonisti juu ya Falastini. Wafalastini hawakuridhia kuundwa kwa makaazi ya kitaifa ya Mayahudi katika nchi yao na "walikataa kujishirikisha na serikali ya namna yoyote watakayoundiwa isipokuwa ile aina ya serikali ya kitaifa itakayoshughulika na mambo yanayowahusu wananchi wa Falastini. "Lakini, kwa ajili ya kuunda ukaazi wa kiuwananchi, jamii ya Mayahudi, walijenga "taifa ndani ya taifa" katika Falastini.

Ujumbe wa Piil ulimaliza maneno yake na kusema kuwa mambo ya Falastini yalivyo, yamefika kikomo kisichotatuka kwa sababu ya "kutokuwa na budi nako kuwili" kumekuwa sasa ni matata yasiyoweza kusuluhishika. Serikali ya Kiingereza haitaweza, kwa upande mmoja, kuzikubali haki za Waarabu wa Falastini kupata uhuru wao na hapohapo kuhakikisha uundaji wa makaazi ya kiuwananchi ya Kiyahudi. Kwahivyo, Ujumbe uliamua kuwa Falastini ipigwe mapande mawili yatakayokuwa huru. Pande moja iwe nchi ya Waarabu wa Falastini na ya pili ya Kiyahudi, na

Jarusalemu iwe chini ya uongozi wa Chama Cha Mataifa.

Pande zote mbili zilipinga mipango hiyo. Wazayonisti walidai kuwa mipango hiyo ilikwenda kinyume na Ilani Ya Balfoo na pia Hukumu Ya Falastini. Wafalastini walikataa kukubali nchi yao kugawiwa na kutayarishwa taifa la Kiyahudi katika sehemu ya nchi yao. Mikutano ya kushauriyana zaidi juu ya mambo haya iliyofanywa London haikufaulu. Hatimaye, mwezi wa Mei 1939 Serikali ya Kiingereza ilitangaza kuwa badala ya kuigawa, Falastini itapata uhuru wake 1949 ikiwa nchi moja ambayo Mayahudi na Waarabu watashirikiana katika kuendesha serikali na utawala. Chama Cha Wazayonisti kilipinga mpango huu. Badala yake, walikutana New York 1942 na kuchagua kuufuata "Mpango Wa Biltimoo" ambao ndani yake ulidai kutayarishwa kwa dola la Kiyahudi katika Falastini.

Kuanzia mwisho wa Vita Vya Pili Vya Dunia Nchi Za Waarabu pamoja na Marekani ziliingia katika majadiliano ya Falastini.

Mnamo 1946, Jopo La Utafiti la Waingereza na Wamarekani, lilitoa maoni mengine tena. Maoni ambayo Serikali Ya Kiingereza iliona kuwa hayatekelezeki. Njia kadha wa kadha za suluhu zilizungumzwa katika mkutano ambao mwishowe haukutoa tijara yoyote. Hatimaye baada ya kutawala Falastini miaka thalathini Serikali Ya Kiingereza, mnamo Februari 1949 iliamua kuukabidhi Umoja Wa Mataifa masiala yanayohusu Falastini. Serikali Ya Kiingereza ilinena kuwa "kukabiliwa na mzozo unaohusu haki isizoweza kutatua . . . [Serikali Ya Kiingereza] imeamua kuwa njia iliyobakia sasa ni kupeleka jambo hilo Umoja Wa Mataifa ili lihukumiwe . . . ."

Baada ya miaka thalathini kufuata Ilani ya Balfoo, na maumbile ya Falastini kugenzwa kwelikweli, Hukumu La Waingereza ndipo lilipofikilia mwisho wa uhakimu wake. Idadi ya Mayahudi ilipanda juu kutoka watu 56,000 katika 1918 hadi watu 608,000 kufikia 1946. Na idadi ya watu wote ikafikia 1,850,000 (angalia Taswira ya 3). Sababu kubwa ya uhamiaji wa Mayahudi Falastini ilitokana na ukatili wa Manatzi juu ya ukhabithi uliowakuta Mayahudi. Lakini, idadi ya uhamiaji wa ghafla namna hiyo ilisababisha shida kuu juu ya umati wa Waarabu wa Falastini. Na, ilivyokuwa Waarabu sio waliowatendea Mayahudi ukatili huo, basi walipinga kulazimishwa kujitolea sadaka nafsi zao. Kama Ujumbe Wa Kifalme unavyokaririia haya:

> "Msemaji hodari juu ya haki za Waarabu alitueleza si kuwa katika historia yao yote hawakuwa na chuki juu ya Mayahudi, bali halikadhalika ni wazi kuwa wao siku zote ni watu wanaopendelea maslaha ya watu wote. Hakuna mwanadamu yoyote yule aliyekuwa na mawazo ya kiutu ambaye hatapendelea kutenda iwezekanavyo kutendwa na mwanadamu ili kuondosha shida na mashaka yanayowakuta

watu hawa /Mayahudi/, iwapo matendo yake mtu huyo hayatakuwa ndio sababu ya kuwatia binadamu wengine katika shida na mashaka kama hayo."

## V. KUPIGWA MAPANDE FALASTINI NA KUUNDWA KWA ISRAELI

Hadi kufikia 1947, Falastini ilikuwa nchi yenye fujo na ukatili mwingi.

Waarabu wa Falastini walipinga, kwa kufanya fujo kali, mipango ya Hukumu iliyoruhusu uhamiaji wa Mayahudi kwa wingi na kupewa watu hao ardhi zilizokuwa za Wafalastini. Hapo awali wageni wa Kiyahudi waliokuja kuhamia Falastini walifuata mafunzo ya Havlaga, yaani kujikanya na kuwa na ustahmilivu. Lakini kufikilia 1947, vyama vya Kizayonisti vyenye maumbile ya kijeshi kama vile Hagana na Irgun, vilianza kutumia ujuzi wao wa silaha. Baadaye wakaunganana na gengi la Stani.

Makundi haya ya maharamia yalianza kutia khofu katika nyoyo za watu kwa kutenda ukatili katika Falastini. Kwa mujibu wa habari rasmi, katika 1940 meli iitwayo Patria iliyopakia wahamiaji waliokuwa maharamia ilizamishwa bandarini na Mayahudi wenziwao waliokuwa nchi kavu na ikawa sababu ya watu 252 kutoweka. Katika 1942, Waziri Wa Mambo Ya Nchi wa Uingereza aliuliwa Kairo na gengi la Stani. Habari rasmi iliyotolewa Uingereza ilieleza mnamo 1944, kuwa "juhudi zilizofanywa na vyama vya kiharamia vilifikilia kilele kipya cha ukatili waliporipua bomu lililobomoa upande mmoja mzima wa Hoteli Ya Mfalme Sulemani huko Jarusalemu." Wafanyi kazi thamanini na sita wa Serikali waliokuwa Waarabu, Mayahudi na Waingereza pamoja na raia watano waliuwawa katika mripuko huo. Falastini ilisemekana kuwa ni boma lililojaa vifaa vya vita.

Umoja Wa Mataifa ambao ndio uliochukua mahali pa Chama Cha Mataifa, ulikuwa na umri wa miaka miwili tu ulipopewa jukumu la kuamua matata ya Falastini. Mnamo mwezi wa Mei 1947, Baraza Kuu la Umoja Wa Mataifa liliunda Tengo Makhsusi Juu Ya Falastini (UNSCOP) na iliwapa nguvu za kuungamanisha masiala yanayohusu Mayahudi wa Ulaya na hiyo Falastini. Haya yalitendwa juu ya kuwa Waarabu wa Falastini na wajumbe wengineo wa Waarabu walipinga mpango huo. Walijadili kuwa nchi nyinginezo pia zipokee umati wa Mayahudi waliohamishwa makwao kwa sababu ya vita. Tengo hilo lilizuru Falastini na nchi nyingine za Waarabu na vilevile Ujarumani na Ostia.

Moja katika lengo la Umoja Wa Mataifa ni kuheshimu kanuni za watu za kujitawala wenyewe. Kanuni hii ilikubaliwa na madola na ilifuatwa katika mambo ya nchi nyingine za Waarabu zilizokuwa chini ya Hukumu ya Chama Cha Madola. Lakini kanuni hiyo haikufuatwa Falastini. Tengo Makhususi Juu Ya Falastini lilizungumza haya katika taarifa yao iliyonena yafuatayo:

". . . Katika wakati wa kuunda Hukumu za awali (kanuni ya watu kujitawala wenyewe) hazikufuatwa tukizingatia Falastini; ni dhahiri kuwa sababu yake inatokana na nia ya kutaka kuunda Makaazi Ya Kitaifa Ya Kiyahudi. Hakika inaweza kusemekana Kuwa Makaazi Ya Kitaifa Ya Kiyahudi na hiyo Hukumu ya aina ya pekee juu ya Falastini zinakwenda kinyume na kanuni hiyo."

Tengo Makhsusi Juu Ya Falastini liliamua kuwa Falastini ipewe uhuru wake bila ya kukawilishwa. Lakini wanachama wa Tengo hilo walikuwa na fikira zilizotafautiana juu ya namna ya uhuru wenyewe. Wachache wao walipendelea Serikali ya muungano lakini kila umati uwe na uwezo mkubwa wa kuendesha majambo yao. Wengi ya wanatengo walipendelea kupigwa mapande na Falastini iwe nchi mbili; moja ya Kiyahudi na ya pili ya Kiarabu na Jarusalemu iwe sehemu ya mataifa yote na iendeshwe na Umoja Wa Mataifa (Mapande yaliyofikiriwa kugawiwa na umati wake, angalia Taswira ya 3 na 4).

Majadiliano marefu juu ya fikira mbili za Tengo yalijadiliwa. Katika mjadala, Umoja Wa Mataifa ilihojiwa vikali iwapo kweli inayo haki ya kugawa mapande Falastini. Mwishowe baada ya kufanywa hila za kichinichini za kisiasa, Baraza Kuu La Umoja Wa Mataifa lilibadilisha kidogo, na kupasisha, mpango wa wengi ya Wanatengo.*

Hukumu Ya Waingereza juu ya Falastini ilikuwa ifikie mwisho wake na kuundwa kwa nchi mbili (moja ya Waarabu, moja ya Mayahudi) ambazo zipate uhuru tarehe 15 Mei 1948.

Azimio La Kupiga Mapande Falastini lilikuwa na mambo mengi ndani yake yenye kukinga haki za walio wachache na "haki zinazokubaliwa sasa" za watu wa dini mbalimbali katika Jarusalemu ambazo zilikuwepo tokea wakati walipotawala Waathumani. Mlikuwemo ndani ya azimio haki za watu wote wa dini mbalimbali kuweza kuzuru mwahala mwa kufanya ibada katika Jarusalemu. Haki hizi zilikuwa ni lazima zipewe umuhimu katika sheria kuu za nchi zote mbili.

Ijapokuwa eneo la taifa walilopewa Mayahudi na Azimiyo La Kupiga Mapande Falastini lilikuwa ni dogo kuliko vile kilivyotaka Chama Cha Wazayonisti lakini Chama hicho kilifuzu katika lengo lake la Kujipatia Taifa La Kiyahudi katika Falastini. Kwa hivyo, Chama Cha Wazayonisti kilikubali mpango wa mapande. Waarabu wa Falastini na Waarabu wa nchi nyingine walilipinga azimio hilo na kusema kuwa si la haki wala si la halali.

---

*Azimiyo 181 (II), la tarehe 29 Novemba 1947, linalojulikana zaidi kama "Azimiyo La Kupiga mapande Falastini."

## Taswira ya 3

(Zingatia: Mayahudi 31.7%
Waarabu 68.3%)

(Zingatia: Mayahudi 56.4%
Waarabu: 42.9% Jarusalemu 0.7%)




## Taswira ya 4




Taifa la Kiyahudi Taifa la Kiarabu Jarusalemu

Idadi ya watu kwa mujibu wa wanachama wengi wa Tengo Makhsusi Juu Ya Falastini (UNSCOP).

Fujo ambalo lilikuwa halijapungua wakati Umoja Wa Mataifa ulipokuwa ukijadili mambo ya Falastini, sasa lilifoka tena upya. Mchafuko ulizidi wakati majeshi ya Uingereza yalipojitayarisha kuondoka, na baadaye walipoamua kuondoka tarehe 15 Mei 1948, mapema zaidi na walivyokusudia awali. Kwa upande mmoja, majeshi ya Wazayonisti yalianza kushambulia ili kuthibiti "Mpango Wa Dalet." Mpango Wa Dalet ulikuwa na lengo la kuteka bila ya kutaakhari, ardi walizopewa Waarabu wa Falastini kuunda Taifa lao waonapo tu kuwa nguvu za Waingereza zimepungua. Lengo la Wazayonisti lilikuwa kuteka ardhi zaidi ili "kufanya Taifa lao kubwa zaidi na la Kiyahudi kwa kutumia nguvu walizonazo Chama Cha Hagana." Kwa upande mwingine, wapiganaji wa Kifalastini pia walizidisha vita vyao. Ukatili ulizidi na walioteswa zaidi ni raia wa Kifalastini.

Katika ukhabidhi uliopindukia mipaka ulitendwa na Wazayonisti walipohujumu kijiji cha Waarabu cha Deri Yasini. Kijiji ambacho kilijaribu kujiepusha na ukatili wa mapigano kilipoteza wanaume, wanawake na watoto 225, waliposhambuliwa na kuuliwa na Wazayonisti. Kisasi kilifuata na Waarabu wakahujumu msafara wa Kiyahudi na kuuwa watu 77. Hofu iliyosababishwa na ukatili wa Deri Yasini iliwafanya Waarabu wa vijiji vingine kuhama ili kukimbiza roho zao.

Tarehe 14 Mei 1948, wakati ambao mapambano yalikuwa yanazidi. Taifa La Israeli lilitangaza kuundwa kwake kwa kufuatia Ilani Ya Belfo, Hukumu Ya Mataifa na Ilani Ya Mapande. Majeshi ya mwisho ya Waingereza yalipoondoka kwa shangwe siku ya pili yake, majeshi ya nchi za Waarabu zilizopakana na Falastini yaliingia katika ardhi walizoahidiwa Waarabu wa Falastini, na huo ndio ulikuwa mwanzo wa vita vya Waarabu na Mayahudi.

Hata kufikia wakati ambao Halmashauri Ya Usalama Ya Umoja Wa Mataifa walipoweza kuzuia mapambano, majeshi ya Waisraeli yalikuwa yamethibiti ushindi. Na zaidi ya hayo yalijuwa yameteka ardhi nyingi zilizoazimiwa kupewa Taifa La Waarabu Wa Falastini, waliteka pia sehemu ya magharibi ya Jarusalemu ambayo ilikusudiwa iwakilishwe na madola ya ulimwengu.

Mipaka iliyokubaliwa ili kusitiza vita mnamo 1949 (angalia Taswira ya 5) ilisababisha Waisraeli kumudu asilimia 67 ya ardhi ya Falastini. Misri na Jodani iliwakilisha sehemu zilizobakia za Taifa La Waarabu Wa Falastini walizopewa na Ilani Ya Mapande. Upote Wa Gaza uliamiriwa na Wamisri na "Kando Ya Magharibi" iliendeshwa na Jodani ambayo katika wakati huo haikuwa mwanachama wa Umoja Wa Mataifa. Katika Mataifa mawili yaliyokusudiwa kuundwa na Ilani Ya Mapande, moja tu liliundwa, nalo ni Taifa La Mayahudi la Israeli. Lakini, la pili, la Waarabu wa Falastini bado halijazalikana.

Taswira ya 5



UN PARTITION PLAN – 1947
AND
UN ARMISTICE LINES – 1949
Boundary of Former Palestine Mandate
PLAN OF PARTITION, 1947
Arab State
Jewish State
Jerusalem
Armistice Demarcation lines, 1949
LEBANON
SYRIA
GOLAN
Tyre
Acre
Haifa
Lake Tiberias
Tel Aviv
Amman
MEDITERRANEAN
SEA
Dead Sea
JORDAN
ISRAEL
El Arish
SINAI
EGYPT
Gulf of Aqaba
The designations employed and the presentation of material on this map do not imply the expression of any opinion whatsoever on the part of the Secretariat of the United Nations concerning the legal status of any country, territory, city or area or of its authorities or concerning the delimitation of its frontiers or boundaries
UNITED NATIONS
ISRAEL
SYRIA
JORDAN
EGYPT

## VI. MASIALA YA FALASTINI KATIKA UMOJA WA MATAIFA, 1948-1967

Ilivyokuwa kutayarisha yaliyokubaliwa katika Ilani Ya Mapande yamekwisha kutanguliwa na mambo yalivyokwenda, Umoja Wa Mataifa ulikuwa sasa na jukumu la masiala ya Falastini. Kwa hakika, mushkili wa kuunda Taifa La Waarabu Wa Falastini bado ungali umebakia. Ijapokuwa kutenda hilo lilikuwa ni lengo la mataifa ya dunia kama ilivyoelezwa na Chama Cha Mataifa mnamo 1919 na baadaye tena na Umoja Wa Mataifa katika 1947, Taifa La Waarabu Wa Falastini bado halijaudwa.

Hatua ya kwanza walioichukua Umoja Wa Mataifa ni kumpeleka Kaunt Folki Benadote wa Swideni kuwa msuluhishi ili "kutafuta njia za suluhu katika mambo yatakayofuata baadaye huko Falastini. Baada ya mapatano marefu na pande zote mbili, alitoa maoni yake ambayo aliyaita "njia za mapatano zenye kukubalika." Maoni yenyewe yalikuwa na mpango wa marakibisho wa mipaka, kuachiliwa kurejea makwao Waarabu wa Falastini waliokimbiza nafsi zao na pia kuzuia kwa kadiri fulani uhamiaji wa wageni wa Kiyahudi Falastini. Benadote aliyapa umuhimu sana mashakili ya wale waliokimbiza roho zao. Mashakili ambayo ndiyo yaliyokuwa kizingiti kikubwa kinachopinga usalama. Alitoa taarifa kuwa Waarabu waliokimbiza roho zao (ambao baadaye walikisiwa na idadi ya watu 726,000) "walikimbia au walifukuzwa kutoka katika sehemu zilizotekwa na Mayahudi." Alitoa mashauri kuwa Umoja Wa Mataifa ukariri "haki za waliokimbiza roho zao kurudi makwao" kwa upesi kama iwezekanavyo, alinena:

> "Itakuwa dhambi kuu juu ya kanuni za Sharia za kibinadamu iwapo hawa waliodhulumiwa na ugomvi huo watanyimwa haki yao ya kurudi makwao, na huku wageni wa Kiyahudi wanaachiliwa kuhamia Falastini, na kukhofisha kuwa watanyakua mahali pa hao Waarabu ambao asili yao tokea enzi na jadi imeanzia katika nchi hiyo."

Benadote alitoa mashauri mengine pia. Lakini kabla ya Umoja Wa Mataifa kuweza kutekeleza lolote juu ya mashauri yake kazi yake katika Falastini ilifikilia kikomo chenye kusikitisha. Tarehe 17 Septemba 1948, Benadote aliuliwa na gengi la Stani.

Mnamo Disemba 1948, Baraza Kuu La Umoja Wa Mataifa lilikariria haki za waliokimbiza roho kurudi makwao.* Pia liliunda Jopo La Kutafuta Suluhu Falastini ili kuamua masiala ya ardhi** waliokimbiza roho zao na

---

*Kumbukumbu Rasmi za Baraza Kuu, Mkutano Wa Tatu Nyomgeza Nambari II (A/648) Taarifa ya Umoja Wa Mataifa Maendeleo Ya Msuluhishi wa Falastini, p. 14.

**Azimio 194 (III) la tarehe 11 Disemba 1948.

mambo yanayohusu Jarusalemu. Katika Mei 1949, Israeli ilipewa uwanachama wa Umoja Wa Mataifa. Kukubaliwa na kuendelea na uwanachama wake kulitegemea kufuata kwake maazimiyo mawili yaliyopasishwa juu ya Falastini--Azimiyo 181 La Kupiga Mapande na azimiyo 194 la Disemba 1948.

Jopo La Kutafuta Suluhu Falastini lilikabili mambo hayo ya Falastini ambayo yamekuwa na matatizo marefu. Na wakati huo Waarabu walionesha kuwa wako tayari kukubali kutafuta suluhu lakini Israeli ilionesha kuwa haikuwa tayari kutoa ngawira walizozipata kutokana na vita. Jopo La Suluhu lilishindwa katika kazi waliyopewa, na mambo yakabakia katika hali hiyo na kuota mizizi kila wakati ukipita. Israeli polepole ilizimeza ardhi ilizoziteka 1948, nchi ambazo zilikuwa nje ya mipaka ya ardhi ilizopewa; hatimaye ardhi hizo zikamilikiwa kabisa na Israeli. Mnamo 1950, Jodani, ambayo bado haikuwa mwanachama wa Umoja Wa Mataifa (ilikuwa mwanachama 1955), iliweka Kando Ya Magharibi Chini ya utawala wake ijapokuwa nchi nyingine za Waarabu zilipinga kitendo hicho. Wakimbizi wa roho zao walibakia ugenini. Katika Disemba 1949, Baraza Kuu La Umoja Wa Mataifa liliunda Diwani Ya Msaada Na Wafanya Kazi Kwa Ajili Ya Wakimbizi Wa Roho Zao Wa Falastini ili kuwasaidia Wafalastini walionyimwa haki za kurudi makwao na njia za kujipatia maisha yao. Diwani hiyo ilipoanza kazi yake 1950, jambo kubwa ililotaka kutenda ni kusaidia mambo yanayohusu chakula, mahala pa kukaa na afya za wakimbizi wa roho zao. Lakini kila wakati ulipopita mambo yanayohusu elimu na kufunza kazi vijana wa Kifalastini yaliangaliwa kwa hali na mali zaidi. Hata kufikilia 1967 ulimwengu uliangalia mambo haya ya Wafalastini kama kwamba ni mambo yanayohusu ukimbizi peke yake.

Lakini wakati wote huo ukweli wa hali ya mambo yanayohusu Falastini yalikuwa yakichipuza. Hali ya ukweli wa mambo yalivyo yalisababisha mgogoro mwingine ambao ulisababisha vita vya pili 1956, baina ya Waarabu na Mayahudi juu ya Mfereji Wa Suezi. Katika 1967, hali ya mambo yalivyo yalitikiswa kwelikweli na vita vya tatu baina ya Waarabu na Mayahudi. Vita vya 1967 vilikuwa sababu ya mambo ya Mashariki Ya Kati kuanza kubadilika. Lakini kitovu cha mgogoro kilikuwa habari ya Wafalastini.

## VII. UTAMBUZI WA HAKI ZA WAFALASTINI ZA KUJITAWALA WENYEWE

Katika vita vya Juni 1967, Israeli ilipanuka kwa kutawala nchi zilizobakia za Waarabu pamoja na Jarusalemu, zilizokuwa chini ya Kukumu Ya Falastini. Pia iliteka Milima ya Golani ya Suuria na Sinai ya Misri (angalia Taswira ya 6).

Vita vya 1967 vilisabibisha umati mkuba wa Wafalastini kukimbiza roho zao mara ya pili. Nusu milioni ya Wafalastini walikimbizwa makwao. Hawa wakimbizi wa roho zao wa vita vya 1967 wanajulikana kama "wakimbizi wapya," nao ni tafauti na wale "wakimbizi wa zamani" wa vita vya 1948. Halmashauri Ya Usalama Ya Umoja Wa Mataifa kwanza iliweza kuzuia vita na kuleta usalama ambao haukuwa na mashiko ya sawasawa. Tena baadaye iliwataka Waisraeli watayarishe mipango ili waliokimbiza roho zao 1967 wapate kurudi makwao,* na kufuata mapatano ya nne yaliyokubaliwa Jiniva (1949) juu ya ardhi zilizotekwa.** Israeli haikufuata hata moja katika haya.

Baadaye Halmashauri Ya Usalama Ya Umoja Wa Mataifa ilipasisha azimio moja ambalo lilikuwa na umuhimu mkuu. Azimio 242 la tarehe 22 Novemba 1967 lilitangaza, utamalakaji wa nchi kwa njia ya vita kuwa jambo hilo halikubaliwi, na Halmashauri hiyo iliwaambia Waisraeli waondoshe askari wake "kutoka katika nchi walizoziteka" katika vita. Azimio lilitaka pia kutishana au vitendo vya kutumia mabavu vikomeshwe. Azimio liliwataka wote waliohusika kukubali kuwa nchi zote zina haki za kitaifa na kuheshimu uhuru wa kila moja katika nchi hizo, na haki ya kila nchi kuishi katika usalama katika mipaka imara iliyokubaliwa. Na zaidi ya hayo, azimio lilidai kuwa waliokimbiza roho zao wapewe haki zao. Israeli ilipinga kutoka katika nchi ilizoziteka kabla ya kupatikana suluhu juu ya mambo yote yaliyokubaliwa katika azimio 242. Ilishikilia uzi huo ingawaje Baraza Kuu La Umoja Wa Mataifa lilikariria maombi yake ya kutaka Israeli waondoke nchi za watu.

Juu ya hayo, haki za Wafalastini juu ya kupata uhuru na nchi yao wenyewe zimefikilia mbali tokea vita vya 1967. Chama Cha Ukombozi Wa Falastini (PLO), kilichoundwa 1964, kilifikilia maafikiano ya mkataba wa kitaifa mnamo 1968. Makubaliano hayo yameahidi kuwa Wafalastini watapigania haki zao. Katika haki hizo ni haki za kujitawala nafsi zao,

---

*Azimio 237 (1967) la tarehe 14 Juni 1967.

**Mapatano haya yalifanywa baada ya Vita Vya Pili Vya Dunia yakiwa na lengo la kuhifadhi haki za wale watu wanaotawaliwa na nguvu za kijeshi.

Taswira ya 6




*TERRITORIES OCCUPIED BY ISREAL, JUNE 1967*

kupata uhuru na utawala wa nchi yao, haki ya waliokimbiza roho zao kurudi makwao na kwenye mali zao huko Falastini, na haki za kutumia vifaa vya vita katika kufikilia lengo hizo.

Mkataba ulisema kuwa Iaraeli ni taifa lisilokuwa la halali, na ulikanusha "azimio zote zinazokwenda kinyume na lengo la kuikomboa Falastini kabisakabisa." Haya yalisabibisha Israeli kukataa kuwa na uhusiano wa aina yoyote na Chama hicho. Makundi ya Wafalastini yaliyokuwa chini ya uongozi wa Chama Cha Ukombozi Wa Falastini kilizidi kutenda vitendo vya fujo* ili kuufanya ulimwengu uangalie vizuri mambo yaliyowakuta Wafalastini na kuujuza ulimwengu kuwa watashikilia kani mpaka wapate haki zao.

Wafalastini walifuzu katika lengo lao la kutaka kukubaliwa na nchi mbalimbali za ulimwengu juu ya haki yao ya hayo wanayoyapigania na kuwa kisa chao ndiyo kiini cha ugomvi uliopo Mashariki Ya Kati. Kukubaliwa huko na ulimwengu kulikaririwa pia katika azimio mbalimbali za Umoja Wa Mataifa.

Ijapokuwa Baraza Kuu La Mataifa huwakilisha kila nchi iliyokuwa mwanachama, lakini Baraza hilo halina nguvu, kama iliyonayo Halmashauri Ya Usalama, ya kuwafanya wanachama kufuata yaliyopasishwa. Na ingawa Halmashauri iliendelea hadi 1967 kusema kuwa tatizo la Falastini "linahusu wakimbizi wa roho zao" lakini mnamo 1969 Baraza Kuu lilielewa kuwa jambo hilo lina matatizo ya kisiasa na kueleza kuwa "asili ya shida zenyewe zinatokana na kunyimwa haki zao zisizokanushika, hao Waarabu wa Falastini. Katika 1970, 1971 na 1972, azimio za Baraza Kuu zilitangaza kuwa inataka iheshimiwe kuwa haki hizi za Wafalastini "ni jambo lenye umuhimu kabisa katika kuweza kupata usalama wenye adili na utakaoweza kudumu katika Masharika Ya Kati."

Mnamo 1974, mataifa ya Kiarabu yalikubali kuwa Chama Cha Ukombozi Wa Falastini peke yake ndiyo wakili rasmi wa watu wa Falastini. Kukiri kwa jodani juu ya jambo hili kulikuwa na umuhimu maalumu kwa sababu tokea 1948 hadi 1967, Jodani iliuwakilisha Ukingo Wa Magharibi (ya mto wa Jodani). Katika orodha ya mkutano wa Baraza Kuu mnamo 1974, mlikuwemo masiala yanayohusu "hoja ya Falastini" kwa mara ya kwanza tokea 1952. Katika mkutano huo wa 1974, Chama Cha Ukombozi Wa Falastini kilipewa wadhifa wa kuhudhuria (bila ya kuingia Katika majadiliyano) ya Baraza Kuu--Chama hicho baadaye kilipewa fursa hiyo katika matawi yote

---

*Walidai kuwa wana haki hiyo kwa kulingana na yaliyokaririwa na Baraza Kuu La Umoja Wa Mataifa lililosema kuwa ni halali kwa watu wanaopigania haki zao za kujigomboa katika ukoloni na kutawaliwa na wageni, kutumia njia yoyote, hata ile ya kutumia vifaa vya vita.

ya Umoja Wa Mataifa. Katika mwaka huohuo, Baraza hili lilitambua kuwa Wafalastini wana haki halisi ya kujitawala wenyewe, kujipatia uhuru wao na nchi yao na kurudi makwao. Baraza lilikubali pia kuwa chama hicho Cha Ukombozi kuwa ndiyo wakili wa Wafalastini, na ni Chama chenye umuhimu mkuu katika makubaliyano yoyote yanayohusu Falastini.

Kutoka 1975, azimio mbalimbali za kila mwaka za Baraza Kuu zimekariria jambo hilo. Na zaidi ya hayo, azimio hizo zimetilia mkazo kuwa hoja ya Wafalastini ni kitovu cha ugomvi wa Mashariki Ya Kati. Na haya ni sawa na kukiri kuwa hapatapatikana usalama wowote katika Masharika Ya Kati bila ya kwanza, kupewa haki zao Wafalastini. Mambo kadhawakadha yanayohusu mgogoro wa Falastini yalizungumzwa na matawi mengine ya Umoja Wa Mataifa yanayohusikana na utawala batili wa Israeli juu ya Kando Ya Magharibi na sehemu ya Gaza. Jopo Lenye Kuangalia Haki Za Binadamu na Tengo Linalohusika Na Matendo Ya Israeli, yaliyowekwa na Baraza Kuu mnamo 1968, yamelaumu kuwa Israeli imewanyima Wafalastini haki zao za kibinadamu. Taarifa zao zimeshambulia vikali Israeli kwa kuzifanya nchi hizo kama mali yake, na kujenga makaazi ya Mayahudi katika ardhi hizo zinazotawaliwa na Israeli; yamelaumu pia unyakuzi na utekaji nyara wa mali za watu, na kuwakamata Wafalastini kuwatendeya sivyo na kuwaadhibu raia hao, kuwafukuza na kutowaruhusu kurudi nchini kwao na kadhalika.

Katika 1975, Baraza pia liliunda Jopo linalohusika na kuangalia haki za Wafalastini. Mara kwa mara Baraza lilikubali na kutilia mkazo maoni ya Jopo hilo ya kutaka Israeli iondoke na kupewa Wafalastini haki zao halisi.

Mwanakiti wa Jopo hilo alisema wazi kuwa ingawa jukumu kubwa la Jopo ni kurekibisha namna watu wanavyoelewa mambo haya ya Falastini kwa sababu ya kusikia zaidi sauti ya upande mmoja, lakini kukubali kwao juu ya haki za Wafalastini hakuhoji kwa namna yoyote Utaifa au kuwepo kwa Israeli, ambayo ni mwanachama kamili ya Umoja Wa Mataifa.

Kwahivyo, kutoka 1974, mataifa mbalimbali katika Umoja Wa Mataifa yalikubali haki iliyomo katika madai ya Wafalastini juu ya kuendesha mustakabali wao na kupata uhuru wao, na kuwa hoja ya Wafalastini ndiyo kiini cha mzozo uliopo Mashariki Ya Kati, na kuwa Chama Cha Kukomboa Falastini ni wakili halali wa Falastini. Mambo haya yalipasishwa pia nje ya Umoja Wa Mataifa, katika maneno ya mkusanyiko wa madola, kama vile madola yasiyofungamana na upande wowote ule, na Umoja Wa Nchi Za Kiafrika. Hivi karibuni nchi za Ulaya Ya Magharibi vilevile zimekubali kuwa Wafalastini wana haki ya kuendesha mustakabali wao.

Juu ya hayo Israeli imeng'ang'ania ardhi za Ufuko Wa Magharibi na Gaza. Inapinga fikira ya kuundwa Taifa La Kifalastini katika ardhi hizi ijapokuwa madola mengi ya ulimwengu yanapendelea jambo hilo kama

tulivyoeleza. Badala yake Israeli inaonesha ishara ya kutaka kuendelea na kuwakilisha utawala wake katika nchi hizo. Katika miaka kadha iliyopita Israeli imezidi kudai kuwa Kando Ya Magharibi ya mto wa Jodani ni mali yake, na inaita ardhi hiyo Judia na Samaria kwa kufuatia majina ya Kibiblia. Israeli imewakamata au kuwafukuza Wafalastini, na kuwanyang'anya mali na ardhi zao ili kujenga miji ya Kiyahudi ya kiraia na ya kijeshi na sababu wanayoitoa ni kulinda usalama wao. Katika nchi hiyo ambayo kuna shida ya maji, Israeli imenyakua sehemu zile zenye maji, Israeli imeendelea mwendo huohuo juu ya kwamba Baraza Kuu na Halmashauri Ya Usalama zimekariria kuwa zinataka mambo hayo yasitizwe. Katika 1979 na mwanzoni mwa 1980, Halmashauri imeilaumu mipango ya Israeli ya kujenga miji ya Mayahudi, na kuona kuwa mipango hiyo ni kizingiti kirefu chenye kupinga mapatano ya Suluhu katika Mashariki Ya Kati na Halmashauri iliunda Tengo la kuchungua na baadaye kutoa taarifa yake juu ya vitendo vya Waisraeli katika nchi walizoziteka.

Tukiangalia nje ya Umoja Wa Mataifa tunaona kuwa mkataba wa suluhu baina ya Israeli na Misri umewatoa polepole Waisraeli katika ardhi ya Sinai ya Misri. Mapatano ya mkutano uliyofanywa katika Kambi Ya Daudi (Marekani) mnamo 1978 baina ya Marekani, Israeli na Misri ulikubaliwa mpango fulani wa kuwapa Wafalastini haki za kuendesha mambo yao wenyewe katika Ukingo Wa Magharibi wa Jodani na Gaza, na huku Israeli iwe na amri juu ya mambo ya kisiasa na ya kijeshi. Wafalastini waliukataa kabisa mpango huo, na kusema kuwa mpango huo unawanyima haki zao za kuendesha mustakabala wao wenyewe, na kuwa mpango huo umefanywa bila ya wao kuwepo na kuwa unakwenda kinyume na matakwa ya Wafalastini. Baraza Kuu La Umoja Wa Mataifa pia limekariria kuwa mpango huo si wa halali.

Mpaka hivi karibuni njia waliyoifuata Halmashauri Ya Usalama ni ile ya azimio 242 (1967) la miaka 13 iliyopita. Lakini, Baraza Kuu, ambalo linaeleza hisiya za madola mengi zaidi, limekiri haki za kimsingi za Wafalastini. Juhudi zilizotekelezwa ili kufanya msimamo wa Halmashauri kuwa unafanana na ule wa Baraza Kuu hazikufuzu. Katika 1976, azimio lenye kusema kuwa Wafalastini wana haki ya kuendesha mustakabala wao ulipasishwa na madola mengi zaidi. Lakini Marekani ilitumia kura yake yenye nguvu za kuzuia chochote kupita, kwa kupinga azimio hilo. Mnamo Agosti 1979, azimio jingine lilipita bila ya kupingwa. Katika Aprili 1980 kulikuwa na mpango mwingine wa kupitisha azimio jengine linalohusu Wafalastini kuendesha mambo yao, lakini Marekani ilitumia kura yake ya nguvu kupinga azimio hilo. Azimio zote hizo zilihalalisha kuwepo kwa Israeli pamoja na mataifa mengine katika sehemu hiyo ya ulimwengu na kuwa nchi hizo zina haki ya utawala wake, usalama, na mamlaka yatakeyoheshimiwa.

Leo Wafalastini wana idadi ya watu milioni nne, idadi kubwa kuliko idadi ya watu katika madola kadhawakadha yaliyo wanachama wa Umoja Wa Mataifa. Kadiri ya nusu milioni ya Wafalastini wanaishi Israeli.

Wengine wenye idadi ya 1,200,000 wanaishi katika ardhi zilizotekwa na Israeli za Kando ya Jordani na Gaza. Waliobakia wamekimbilia nchi nyingine; wengi pia wamo katika kambi za waliokimbiza roho zao, wengi wakiwa ni wageni katika nchi za watu. Wengi zaidi ya hao waliokuwa nje wanatarajia kurudi katika nchi yao.

Bingwa Arnold Tonibii katika maelezo yake ya 1968 aliandika kiini cha ukweli wa hoja hii ya Falastini; alieleza yafuatayo:

> "Katika muda wote huu wa miaka thalathini, Uingereza uliruhusu kuingia Falastini, mwaka baada ya mwaka, kadiri maalumu ya Mayahudi, kadiri ambayo ilibadilika kwa mujibu wa nguvu za Waarabu au Mayahudi /wanaopendelea lengo fulani/ wa wakati huo. Hawa wahamiaji wasingeweza kuingia Falastini ingelikuwa hawakuachiliwa na kuhamiwa na Waingereza. Ingelikuwa Falastini imebakia chini ya utawala wa Waathumani wa Kiturki, au ingelikuwa imekuwa nchi huru ya Waarabu mnamo 1918, wahamiaji wa Kiyahudi wasingelíruhusiwa kuhamia Falastini kwa wingi hata mwishowe wakaweza kuwashinda nguvu Waarabu na kuiteka nchi hiyo ya Waarabu. Sababu kubwa ya kuwa leo Nchi Ya Israeli ipo na sababu ya kuwa leo milioni moja na nusu ya Waarabu wa Falastini ni wakimbizi wa roho zao ni kuwa, kwa muda wa miaka thalathini, uhamiaji wa Mayahudi uliwaelemea Wafalastini kwa kutumia nguvu za majeshi ya Uingereza hata ukafika wakati ambao wageni wakawa ni wengi wa kutosha na wenye nguvu za silaha kuweza kujitetea wenyewe kwa vifaru na ndege zao wenyewe. Msiba wa Falastini si msiba wa mahali padogo tu: ni msiba wa Dunia nzima, kwa sababu ni haramu ambayo inaleta matatizo juu ya usalama wa Dunia."

Umoja Wa Mataifa umeng'amua kuwa jambo lililo muhimu la kuondosha matatizo haya ya usalama wa dunia ni kuwapa Wafalastini haki zao za kuendesha mustakabali wao, kuwa na uhuru wao, na mamlaka huko Falastini.

## TRANSLATION OF FIGURES 1, 5, AND 6

| | | |
|---|---|---|
| al-Arish | = | al-arishi |
| Amman | = | Amani |
| Arab Jaffa | = | Jafa Ya Waarabu |
| Arab State | = | Taifa La Waarabu |
| Beirut | = | Beruti |
| Damascus | = | Damaskas |
| Dead Sea | = | Bahari Mfu |
| EGYPT | = | MISRI |
| El-Arish | = | al-Arishi |
| GAZA | = | Gaza |
| Golan | = | Golani |
| Gulf of Suez | = | Ghuba ya Suezi |
| Gulf of Aqaba | = | Ghuba ya Akaba |
| Hadera | = | Hadera |
| Haifa | = | Haifa |
| ISRAEL | = | ISRAELI |
| JORDAN | = | JODANI |
| Kefa Sava | = | Kafri Sabaa |
| Lake Tiberias | = | Ziwa Tabariya |
| LEBANON | = | LEBANANI |
| MEDITERENIAN SEA | = | Bahari Ya Mediterenіani |
| Nahariyya | = | Nahariva |
| Nawa | = | Nawa |
| Netanya | = | Netanva |

| | | |
|---|---|---|
| PALESTINE | = | FALASTINI |
| Quneitra | = | Kunetra |
| Rafah | = | Rafaha |
| Red Sea | = | Bahari Nyekundu |
| Rehovot | = | Rehovoti |
| Rishon Le Zion | = | Rishoni Ya Zioni |
| Safad | = | Safadi |
| SAUDI ARABIA | = | SUUDIA |
| Sidon | = | Saidani |
| SINAI | = | SINA |
| SYRIA | = | SHAMU |
| SYRIAN ARAB REPUBLIC | = | JAMHURI YA SUURIA YA KIARABU |
| Tel Aviv | = | Telavivu |
| Tiberias | = | Tabariya |
| TRANSJORDAN | = | JODANI KUU |
| Tyre | = | Tairi |
| Figure 1 | = | Taswira ya 1 |
| Figure 5 | = | Taswira ya 5 |
| Figure 6 | = | Taswira ya 6 |
| ARMISTICE DEMARCATION LINES, 1949 | = | MIPAKA YA KUZUIA VITA, 1949 |
| (shown where varience with Mandate boundary) | = | (imechorwa katika sehemu zinazotafautiana na mipaka ya kuzuia vita) |

| | | |
|---|---|---|
| BOUNDARY OF FORMER PALESTINE MANDATE PLAN OF PARTITION, 1947 | = | MIPAKA YA FALASTINI KWA MUJIBU WA MPANGO WA MAPANDE, 1947 |
| Gray area midicates the "Palestine" claimed by World Zionist Organization 1919 | = | Sehemu za kijivu zinaonesha ardhi za "Falastini" zilizo-daiwa na Chama Cha Wazayonisti Wa Dunia mnamo 1919 |
| "PALESTINE" CLAIMED BY ZIONIST ORGANIZATION, 1919 (Source: Ruedy in Abu Lughod: <u>The Trasformation of Palestine</u>) | = | "FALASTINI" ILIYODAIWA NA CHAMA CHA WAZAYONISTI, 1919 (Kutokana na: Rudi katika Abu Lughod: <u>The Trasformation of Palastine</u>) |
| TERRITORIES OCCUPIED BY ISRAEL, JUNE 1967 | = | ARDHI ZILIZOTEKWA NA ISRAELI, 1967 |
| U.N. Peace-keeping Forces | = | Majeshi ya Kuweka Usalama ya Umoja Wa Mataifa |
| The designation employed and the presentation of material on this map do not imply the expression of any opinion whatsoever on the part of the Secretariat of the United Nations concearning the legal status of any country, territory, city or area or of its | = | Majina yaliyotumiwa na namna ya maelezo yalivyoelezwa katika ramani hayaelezi hisiva za namna yoyote za Ofisi Ya Karani Mkuu Wa Umoja Wa Mataifa kuhusu haki za kisheria juu ya nchi ardhi, mji wowote au uwakili wake juu ya sehemu au mipaka. |

authority or concearning the
delimitation of its frontiers
or boundaries.

| | | |
|---|---|---|
| U.N. ARMISTICE LINES - 1949 | = | MIPAKA YA KUSITIZA VITA YA UMOJA WA MATAIFA - 1949 |
| AND | = | NA |
| U.N. PARTITION PLAN - 1947 | = | MPANGO WA MAPANDE WA UMOJA WA MATAIFA - 1947 |